Kioo cha Lugha, Juz. 24(1), 50-70
Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v24i1.4

Ulinganishaji wa Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu Kimofolojia

Dieudonné Butoyi[1], *Dunlop Ochieng*[2], *Zelda Elisifa*[3]

Ikisiri

Makala hii inalinganisha Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu ikilenga kubainisha upekee wa kimofolojia wa Kiswahili cha Bujumbura. Data zilikusanywa kutoka kwa watoataarifa thelathini (30) wa maeneo ya mji wa Bujumbura (Buyenzi) na mkoa wa Kivu Kusini (Bukavu). Mbinu za usaili na ushuhudiaji zilitumiwa na watafiti katika kukusanya data. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa maumbo ya maneno ya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu yanafanana kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, Kiswahili cha Bujumbura kina sifa mbalimbali za kipekee za kimofolojia kama vile kutotumia viambishi vya udogoshaji {bu-} na {hi-} vinavyopatikana katika Kiswahili cha Kivu. Pia, katika muundo wa vitenzi, Kiswahili cha Bujumbura hakihusishi ufupishaji wa kiwakilishi cha nafsi wala kukitumia badala ya kiambishi cha nafsi. Kuhusu kanuni za kimofosintaksia, imebainika kuwa, katika Kiswahili cha Bujumbura, uwiano wa nomino na vitenzi au nomino na vivumishi lazima usimamiwe na viambishi ngeli kutokana na ngeli ya nomino husika ilhali Kiswahili cha Kivu huweza kudondosha viambishi hivyo vyenye dhima ya kuoanisha maneno katika tungo. Kutokana na matokeo hayo, ni dhahiri kuwa Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu huwa na unasaba mkubwa wa kimofolojia.

1.0 Utangulizi

Kiswahili ni lugha ya Kibantu ambayo chimbuko lake ni upwa wa Afrika Mashariki (Massamba na wenzake, 2009). Lugha hii ilienea katika maeneo na nchi nyingi za

[1] Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Lugha na Tamaduni za Kiafrika Chuo Kikuu cha Burundi, Burundi. Baruapepe: dieudonne.butoyi@ub.edu.bi

[2] Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Isimu na Taaluma za Fasihi, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tanzania. Baruapepe: dunlop.ochieng@out.ac.tz

[3] Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Isimu na Taaluma za Fasihi, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tanzania. Baruapepe: zelda.elisifa@out.ac.tz

ulimwenguni, hasa Afrika Mashariki na Afrika ya Kati. Hivyo, Kiswahili kilitambulika kama chombo muhimu cha mawasiliano kwa raia wa maeneo hayo yakiwamo nchi ya Burundi na Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Katika muktadha wa Burundi, Kiswahili kililetwa na Wazanzibari waliokuwa wamefika katika upwa wa Ziwa Tanganyika kwa ajili ya biashara ya utumwa, miaka ya 1800 (Benabou, 1982; Mazunya na Habonimana, 2010; Ntiranyibagira, 2017). Baada ya miaka ya 1850, Kiswahili kilienea katika sehemu mbalimbali za nchi, hasa mijini na kwenye mipaka ya Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambako Uislamu nao ulichangia katika uenezaji wa Kiswahili kwani kilitumiwa kama lugha ya ibada na sala mbalimbali (Nsabimana, 1988; Bizongwako, 1985; CRELACS, 2023; Muaka, Nduwamahoro na Butoyi, 2024).

Kutokana na upana wa maeneo ya Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambako Kiswahili kinazungumzwa, kumedhihirika tofauti za kiisimu, hasa tofauti za kifonolojia, kimofolojia, kimofofonolojia na kimsamiati katika Kiswahili hicho (Nassenstein na Shinagawa, 2019). Kwa mujibu wa wanazuoni hao, hali hiyo ilichochea kutambulika kwa lahaja za Kiswahili cha Kongo ambazo ni Kiswahili cha Kivu, Kiswahili cha Bunia, Kiswahili cha Kisangani na Kiswahili cha Lubumbashi. Tofauti hizo za kiisimu ambazo ni msingi wa ubainishaji wa lahaja hizo, zilishughulikiwa na wanaisimu mbalimbali ili kuonesha utofauti baina yake na kuhakikisha kuwapo kwake (Goyvaerts, 2007; Ferrari na wengine, 2014; Nassenstein, 2015; Bose na Nassenstein, 2016; Nassenstein na Bose, 2016; Nassenstein na Bose, 2020; Nassenstein na Gerrit, 2020). Kwa mfano, sifa za kimofosintaksia za Kiswahili cha Kivu zilichunguzwa na Bose na Nassenstein (2016) ilhali sifa za kinyakati na hali za Kiswahili hicho zilichunguzwa na Goyvaerts (2007). Aidha, viambishi vinavyowakilisha wingi katika Kiswahili cha Bunia vilichunguzwa na Nassenstein (2017).

Lahaja hizo za Kiswahili cha Kongo zilitambulika na kufanyiwa utafiti kwa ajili ya kubainisha sifa za kiisimu zinazotofautisha moja na nyingine. Hata hivyo, hakuna utafiti uliolinganisha hata moja ya lahaja hizo na Kiswahili kinachozungumzwa nchini Burundi wakati baadhi ya sehemu za maeneo ya Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kunakozungumzwa Kiswahili zinapakana. Kwa namna ya pekee, hakuna utafiti uliofanyika ili kuchunguza ufanano na utofauti wa kiisimu baina ya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu. Hivyo, lengo la utafiti huu ni kulinganisha mofolojia ya Kiswahili cha Bujumbura na cha Kivu ili kuona ikiwa kuna upekee wowote wa kimofolojia wa Kiswahili cha Bujumbura.

2.0 Mapitio ya Maandiko

Watafiti kadhaa wamelinganisha lahaja mbalimbali za Kiswahili na lugha zingine, wakilenga kutambua tofauti za kiisimu (kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, kimaana na kimsamiati) baina ya lahaja au lugha hizo. Kuhusu mfumo wa

kifonolojia, Salum (2018) alilinganisha fonolojia za Kitumbatu na Kimakunduchi ambazo ni lahaja za Kiswahili. Mtafiti aligundua mlingano wa silabi zenye sifa ya kudondosha fonimu, usilimisho wa matamshi ya fonimu na kuimarisha na kudhoofisha matamshi ya fonimu. Kuhusu tofauti au ufanano wa kisintaksia, Nyandago (2013) alifanya uchanganuzi linganishi wa sintaksia ya sentensi shurutia ya Kiswahili sanifu na lugha ya Ekegusii. Utafiti huu umebainisha kuwa sintaksia ya sentensi sharti ya Kiswahili sanifu na ile ya lugha ya Ekegusii zinafanana kwa kiwango kikubwa. Utafiti umebaini kuwa lugha hizi mbili zina sentensi sharti zenye miundo ya sentensi changamano, ambapo kishazi shurutiwa ndicho kishazi kikuu na kishazi sharti kikiwa ndicho kishazi tegemezi. Kwa mujibu wa mpangilio wa vishazi kama viambajengo vya sentensi sharti, vishazi shurutiwa vinatangulia vikifuatwa na vishazi sharti.

Kwa upande wa msamiati, Ali (2015) alichunguza tofauti za msamiati wa lahaja ya Kipemba cha kaskazini na Kipemba cha kusini. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha tofauti za msamiati kati ya Kipemba cha kaskazini na cha kusini. Tofauti kubwa iliyoripotiwa ni kuwa Kipemba cha kaskazini kina msamiati wa Kipemba cha zamani ilhali Kipemba cha kusini hukaribiana na Kitumbatu, lakini pia kikielekea kufanana na Kiswahili sanifu kwa kiasi kikubwa.

Aidha, zipo pia tafiti zilizolenga kutambua ufanano na utofauti wa kimofolojia baina ya lahaja au lugha tofauti. Kwa mfano, Salim (2018) alifanya utafiti ambao unadhihirisha mwachano wa kimofolojia baina ya Kiswahili sanifu na Kipemba. Utafiti wake ulibainisha mwachano katika viambishi njeo uyakinishi kwa wakati uliopita (-li-><-e-: alipita ><epite, tulipita><twepita), wakati mtimilifu (-me-><-n(a)-: amepita><kanpita, tumepita><tunpita) na wakati uliopo (-na-><-a-: anapita><apita, tunapita><twapita) na mwachano katika viambishi njeo ukanushi kwa wakati uliopita (-ku-><-e-: sikulima><selima, hatukulima><hatwelima). Pia, ulibainisha mwachano katika matumizi ya kiambishi njeo cha wakati ujao kwenye nafsi ya kwanza katika wakati ujao, ambapo kiambishi nafsi {ni-} hudondoka na kiambishi cha wakati ujao {ta-} kupata mpumuo katika Kipemba (nitasoma><t^{h}asoma, nitalima><t^{h}alima). Vilevile, utafiti huo ulishugulikia mwachano katika uwasilishaji na matumizi ya viambishi nafsi ambapo kiambishi cha nafsi ya kwanza {ni-} huwakilishwa na kiambishi {hi-} kinachowakilisha pia kiambishi cha hali ya kuendelea kwa tendo {ki-} (nikiiba><hiiba, nikifahamu><hifahamu).

Nao Nshimirimana na wenzake (2022) walishughulikia muundo wa nomino ya Kiswahili na nomino ya Kirundi wakichunguza ufanano na utofauti wa matumizi ya ngeli za nomino na dhima ya viambishi ngeli vinavyotokana na utawala wa kimofosintaksia unaotokana na nomino. Hatimaye wamedhihirisha uhusiano baina ya maneno yaundayo tungo, kuwa mfumo wa nomino za Kiswahili unatofautiana kwa kiwango kikubwa na ule wa nomino za Kirundi.

Kwa ujumla, tafiti tangulizi zimejikita katika kulinganisha lahaja za lugha au lugha na nyingine ili kutambua ufanano na utofauti wa kiisimu baina ya hizo

lahaja au lugha. Tafiti hizo zimeshughulikia ufanano na utofauti wa kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, msamiati na maana; na zilihusu hasa lahaja za Kiswahili za pwani na Kiswahili sanifu. Hii inamaanisha uhaba wa tafiti zilizolenga kubainisha lahaja za maeneo mengine hasa katika Afrika ya Kati ambako nako lugha ya Kiswahili inatumika. Kimahususi, ubainishaji wa lahaja haujawahi kufanyika katika Kiswahili kinachotumiwa nchini Burundi. Kwa mantiki hiyo, utafiti huu ulinuia kulinganisha Kiswahili cha Bujumbura kinachozungumzwa mjini Bujumbura nchini Burundi na Kiswahili cha Kivu ambacho ni mojawapo ya lahaja mahususi zilizokwishabainishwa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Matokeo ya utafiti huu yanaimarisha historia na maendeleo ya lugha ya Kiswahili kwa kuongeza maarifa zaidi juu ya kuenea na kubadilika kwa Kiswahili.

3.0 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili ambazo ni Nadharia ya Mwachano na Makutano ya Lugha za Kibantu iliyoasisiswa na Massamba (2007) na Nadharia ya Uchunguzi Linganishi wa Kategoria Dhanifu ya Novakova (2010). Nadharia ya Mwachano na Makutano ya Lugha za Kibantu ilifafanuliwa na kujengwa juu ya nadhariatete ya ndugu na ndugu wa mbali. Kwa mujibu wa nadhariatete hii, lugha za Kibantu zenye unasaba mmoja zinaweza kuwa ni A, B, C, D, na E. Katika mchakato wa makutano, A na B, B na C, C na D, na D na E huweza kuunda jozi za ndugu. Katika muktadha huo, B huwa ndugu wa A na C, C wa B na D, D wa C na E. Kukizingatia uelewa baina ya A na B, B na C, C na D, na D na E, jozi yoyote hujengwa na ndugu. Kwa upande mwingine, A na C, B na D, C na E hujenga jozi ya ndugu wa mbali. Hii ina maana kuwa, kwa mujibu wa nadhariatete hii, mwathiriano baina ya jamiilugha mbili zenye uhusiano wa kinasaba na ambazo zina mawasiliano ya karibu (ndugu) una haki ya kujitokeza zaidi kuliko mwathiriano baina ya lugha za jamiilugha zisizo na uhusiano huo wa kinasaba wala mawasiliano ya karibu (ndugu wa mbali). Hivyo, Nadharia ya Mwachano na Makutano ya Lugha za Kibantu imetumiwa ili kupima undugu baina ya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu.

Kwa upande mwingine, Nadharia ya Uchunguzi Linganishi wa Kategoria Dhanifu ilitumiwa kwa kufuata hatua tatu ambazo ni: (1) kuchagua na kueleza kategoria za kisarufi zitakazohusishwa na ulinganishaji, (2) kueleza na kulinganisha mikakati ya kimofosintaksia inayohusika katika kueleza kategoria zinazohusishwa na ulinganishaji, na (3) kubainisha ufanano na tofauti za kimatumizi baina ya kategoria zinazohusishwa na ulinganishaji. Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi wa Kategoria Dhanifu ilitumiwa kama kigezo muhimu cha kiisimu kwa kulinganisha kategoria teule za Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu na kutambua utofauti na ufanano baina ya aina hizo za Kiswahili, kwa ajili ya kutambua undugu baina yake na, hivyo, kudhihirisha upekee wa kimofolojia wa Kiswahili cha Bujumbura.

4.0 Mbinu za Utafiti

Utafiti wowote unafanyika ukiwa na malengo yanayotarajiwa kufikiwa na, kama ilivyokwishaelezwa, lengo la utafiti huu ni kulinganisha Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu kimofolojia ili kutambua upekee wa kimofolojia wa Kiswahili cha Burundi. Data zilipatikana kutoka kwa watoataarifa wa Burundi kutoka tarafa za Buyenzi jijini Bujumbura na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo eneo la Bukavu mkoa wa Kivu Kusini.

Watoataarifa 15 walichaguliwa kutoka katika kila eneo miongoni mwa maeneo yaliyolengwa na utafiti huu (Buyenzi, Bukavu). Hivyo, jumla ya watoataarifa 30 walishiriki katika kujibu maswali ya hojaji. Usampulishaji usio nasibu ulitumika ili kuwapata watoataarifa ambao wanazungumza Kiswahili katika eneo teule. Watoataarifa hao walihusika katika kusimulia hadithi au habari fupifupi juu ya maisha yao, huku wakirekodiwa na watafiti ili kupata data za kimofolojia zinazohusiana na kategoria za maneno zilizochukuliwa kama msingi wa uchambuzi katika makala hii. Pia, taarifa za habari kumi (10), masimulizi matano (5) na hotuba mbili (2) zilizorekodiwa kutoka katika vipindi mbalimbali vya redio zinazosikika katika eneo la utafiti zilichunguzwa na watafiti kwa ajili ya kupata data; na zoezi hili lilihusika katika kujaziliza data za uwandani.

Mbinu ya usaili na mbinu ya usikilizaji makini pia zilitumiwa na watafiti. Wasailiwa walirekodiwa ili kupata data za kimofolojia ambazo zilipitiwa na watafiti kwa ajili kubainisha ufanano na utofauti kati Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu, na hivyo, kutambua na kubainisha upekee wa kimofolojia wa Kiswahili cha Bujumbura. Katika zoezi hilo la uchanganuzi wa data, watafiti walipanga data katika majedwali kutokana na maeneo zilikotoka. Pia, watafiti walichambua maumbo ya maneno na kuyalinganisha ili kuelewa ufanano na utofauti wa kimaumbo baina ya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu na, hivyo, kutambua upekee wa kimofolojia wa Kiswahili cha Bujumbura.

5.0 Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inahusu uchanganuzi na ufafanuzi wa data. Baada ya kukusanywa kutoka maeneo tofauti, data hizo zilifafanuliwa kwa kulinganishwa ili kubainisha ufanano na utofauti wa kimofolojia baina ya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu na, hivyo, kujaribu kuona ikiwa kuna upekee wowote wa kimofolojia wa Kiswahili cha Bujumbura. Ufafanuzi wa data ulilenga hasa muundo wa nomino na vitenzi pamoja na sifa za kimofosintaksia zinazojitokeza maneno yanapoungana katika tungo au sentensi.

5.1 Muundo wa Nomino katika Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu

Katika lugha za Kibantu, nomino ni kategoria ya maneno ambayo yanaweza kuwa na miundo tofauti kutokana na lugha. Hivyo, muundo wa msingi wa nomino unaweza kuwa wa (1) kiambishi ngeli na shina (mf. Kiswahili: *mtu {m-tu}*), (2) sauti tangulizi, kiambishi ngeli na shina (mf. Kirundi: *umuntu {u-mu-ntu}*), na (3) kiambishi ngeli cha pili, kiambishi ngeli cha kwanza na shina (mf. Lingala: *bandeko: {ba$_2$-n$_1$-deko}*) (Mutaka na Tamanji, 2000). Katika lugha ya Kiswahili, muundo wa msingi wa nomino ni ule wa kiambishi ngeli na shina. Hivyo, ngeli za nomino katika Kiswahili hukamilisha muundo wa nomino kwa kudhihirisha idadi (umoja na wingi) na hali ya udogo na ukubwa.

5.1.1 Viambishi Ngeli Vinavyotumika katika Kiswahili cha Bujumbura

Kama kawaida ya Kiswahili, katika Kiswahili cha Bujumbura, nomino zilitambulika kuwa na muundo uleule wa Kiswahili ambao unashirikisha kiambishi ngeli na shina ili kuunda nomino kamili. Lifuatalo ni jedwali la viambishi ngeli vinavyoshiriki katika muundo wa nomino za Kiswahili cha Bujumbura.

Jedwali Na. 1: Viambishi Ngeli vya Nomino katika Kiswahili cha Bujumbura

	Kiswahili cha Bujumbura	**Mifano**
1.	mu-/mw-/m-	mutu,
2.	ba-/(wa-)	batu, (watu)
3.	mu-	muti,
4.	mi-	miti,
5.	ji-/ø-	jicho, darasa
6.	ma-	macho, madarasa
7.	ki-	kisu
8.	bi-/(vi-)	bisu (visu)
9.	N-	nyumba
10.	ma-/(N-)	manyumba (nyumba)
11.	ru-/u-	(r)urimi (urimi)
12.	ka-/(ga-)	katoto, (gatoto)
13.	tu-/(du-)	tutoto, (dutoto)
14.	bu-/(u-)	budongo
15.	ku-	kukula
16.	-	-
17.	ku-	ku nyumba
18.	mu-	mu kanisa

Chanzo: Uwandani (2025)

Jedwali Na. 1 hapo juu linaonesha viambishi ngeli vinavyofanya kazi katika Kiswahili cha Bujumbura vikishirikiana na mashina ili kuunda nomino kamili katika umoja au wingi. Kwa mfano, nomino *kisu/bisu (visu)* {*ki*-su/*bi(vi)*-su}, rurimi/ndimi {*ru*-rimi/*N*-rimi} na *katoto/tutoto (dutoto)* {*ka*-toto/*tu(du)*-toto} zimeundwa kwa viambishi ngeli {*ki*-} na {*bi(vi)*-}, {*ru*-} na {*N*-}, na {*ka*-} na {*tu(du)*-} na mashina {-su}, {-rimi} na {-toto}.

5.1.2 Viambishi Ngeli Vinavyotumika katika Kiswahili cha Kivu

Katika Kiswahili cha Kivu, nomino inaundwa na kiambishi ngeli na shina. Viambishi ngeli vinavyoshirikiana na shina huwa na dhima ya kuonesha umoja na wingi. Jedwali lifuatalo linaonesha idadi na mfuatano wa ngeli za nomino katika Kiswahili cha Kivu.

Jedwali Na. 2: Viambishi Ngeli vya Nomino katika Kiswahili cha Kivu

	Kiswahili cha Kivu	**Mifano**
1.	mu-/ ø-	mutu, soda
2.	ba-	batu, basoda
3.	mu-	muti,
4.	mi-	miti,
5.	li-/ø-	licho, shamba
6.	ma-	macho, mashamba
7.	ki-	kitu,
8.	bi-	bitu,
9.	ø-/(i)N-	inchi,
10.	(i)N-	inchi,
11.	lu-/u	lupango,
12.	ka-	katoto,
13.	tu-	tutoto,
14.	bu-	bunyumba
15.	ku-	kuliya,
16.	-	-
17.	ku-	ku soko
18.	mu-	mu nyumba
19.	(h)i-	(h)indege, (h)ibusingizi

Chanzo: Uwandani (2025)

Jedwali Na. 2 hapo juu linaonesha viambishi ngeli vinavyoungana na mashina ya nomino katika Kiswahili cha Kivu. Kama ilivyo katika lugha za Kibantu kwa ujumla, viambishi hivyo hutangulia mashina kama vile katika *mutu/batu* {*mu*-tu/*ba*-tu}, mukate/mikate {*mu*-kate/*mi*-kate}, nyumba/manyumba {*N*-umba/*ma*-N-

umba}. Katika mifano hiyo, viambishi ngeli {*mu-*} na {*ba-*}, {*mu-*} na {*mi-*} na {*N-*} na {*ma-*} vimeshirikiana na mashina {-tu}, {-kate} na {-umba} katika kujenga nomino na kudhihirisha idadi (umoja au wingi).

5.1.3 Ulinganishaji wa Miundo ya Nomino za Kiswahili cha Kivu na Kiswahili cha Bujumbura

Kutokana na yaliyooneshwa katika majedwali Na. 1 na Na. 2, katika muundo wa nomino, kigezo linganishi kimeonesha kuwa viambishi ngeli vya Kiswahili cha Bujumbura na vile vya Kiswahili cha Kivu hufanana na kutofautiana kwa kiasi fulani ama kimuundo au kidhima. Kwanza kimuundo, kuanzia ngeli ya 1 hadi ngeli ya 10 ({*mu-, ba-, mu-, mi-, ji-, ma-, ki-, bi-, N-, N-*}) kuna ufanano mkubwa baina ya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu. Hata hivyo, kuna tofauti katika ngeli ya 2 {*ba-*} (mf.: *batu, batoto*) na ya 8 {*bi-*} (mf. *bitu, bisu*) ambapo viambishi ngeli huwa {*wa-*} (mf. *watu*, *watoto*) na {vi-} (mf. *vitu, visu*) kwa baadhi ya Waswahili wa Bujumbura kama vile wanafunzi na wasomi kutokana na athari ya Kiswahili sanifu kinachofundishwa kwenye shule na vyuo. Vilevile, ufanano umedhihirika baina ya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu ambapo viambishi ngeli vya ngeli za 17 ({*ku-*}) na 18 ({*mu-*}) huwa vilevile kwa Kiswahili cha Bujumbura na cha Kivu.

Hata hivyo, baadhi ya viambishi ngeli vya Kiswahili cha Bujumbura vinatofautiana na vile vya Kiswahili cha Kivu kimuundo. Ngeli ya 5 ya Kiswahili cha Bujumbura haitumii kiambishi {*li-*} cha ngeli ya 5 katika Kiswahili cha Kivu (mf. *licho, litawi*). Pia, kiambishi cha ngeli ya 10 ({*ma-*}) katika Kiswahili cha Bujumbura (mf. *manyumba*), ambayo ni wingi wa ngeli ya 9 ({*N-*}) (mf. *nyumba*) hujitofautisha na kiambishi ngeli {*(i)N-*} cha ngeli ya 10 ambayo ni wingi wa ngeli ya 9 ({*(i)N-*}) katika Kiswahili cha Kivu. Vilevile, kiambishi ngeli cha ngeli ya 19 ({*hi-*}) ambacho kinapatikana katika Kiswahili cha Kivu (mf. *hindege, himayi, himbuzi*) hakifanyi kazi katika Kiswahili cha Bujumbura.

Pili, kwa kuzingatia dhima ya viambishi ngeli, kwa kawaida, viambishi hivyo hushikishwa katika mashina ya nomino ili kuikamilisha nomino kiidadi (umoja/wingi) au kuonesha hali zingine za nomino kama udogo na ukubwa wa kitu. Kwa kuzingatia mambo haya mawili, viambishi vya ngeli huhusika katika Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu kuonesha umoja na wingi wa nomino kwa namna sawa. Hivyo, viambishi ngeli vya ngeli ya 1 na ya 2 ({*mu-ba*}), ya 3 na ya 4 ({*mu-mi*}), ya 5 na ya 6 ({*ji-ma*}), ya 7 na ya 8 ({*ki-bi*}) hujenga umoja na wingi kwa namna sawa katika Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu. Hivyo, nomino *mutu* huwa *batu, mukate* huwa *mikate, jina* huwa *majina* na *kisu* huwa *bisu*.

Vilevile, nomino za baadhi ya ngeli hufanya wingi kwa kukopa viambishi kwenye ngeli zingine, na hali hii hutokea ama katika Kiswahili cha Bujumbura au Kiswahili cha Kivu. Hivyo, katika Kiswahili cha Bujumbura, kiambishi cha ngeli ya 11 ({*ru-*}) hufanya wingi katika ngeli ya 10 ({*N-*}) (mf. rurimi><ndimi,

rubao><mbao). Vilevile, ngeli hiyohiyo ya 11 {*(l)u-*} ya Kiswahili cha Kivu hufanya wingi katika ngeli ya 10 ({*N-*}) (mf. (l)ulimi><ndimi, (l)ubao><mbao). Katika kudhihirisha udogo wa nomino, Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu huwa na mfanano kwani viambishi ngeli vya ngeli za 12 na 13 ndivyo vinavyoshikishwa kwenye mashina ili kutunga nomino zinazoashiria udogo au ukubwa wa kitu. Hivyo, katika Kiswahili cha Bujumbura, kiambishi ngeli cha ngeli ya 12 {*ka-*} hutumika kuonesha hali ya udogo katika umoja, ilhali kile cha ngeli ya 13 {*tu-*} huwa wingi wake (mf. *katoto><tutoto, kanyumba><tunyumba*). Katika Kiswahili cha Kivu, hali hiyo hujitokeza hivyohivyo kwani viambishi ngeli vya ngeli za 12 {*ka-*} na 13 {*tu-*} hutumika kuonesha udogo katika umoja na wingi.

Hata hivyo, katika kuunda maneno yenye hali ya kudogosha, zipo tofauti baina ya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu. Hivyo, katika Kiswahili cha Kivu, kiambishi cha ngeli ya 19 {*hi-*} ambayo haipatikani katika Kiswahili cha Bujumbura hushirikiana na mashina ili kudhihirisha udogo (au uchache) usio wa kawaida (mf. *ndege><hindege, mayi><himayi*). Vilevile, katika Kiswahili cha Kivu, kiambishi cha ngeli ya 14 ({*bu-*}) hutumika kuunda nomino kikiwa na mofimu ya udogoshaji na udunishaji (mf. *ngoma><bungoma, nyumba><bunyumba, dagara><budagara*). Tofauti na hiyo, katika Kiswahili cha Bujumbura hali hiyo inajitokeza kama athari ya Waswahili kutoka Kivu kwa Waswahili wa Bujumbura. Kwa upande mwingine, Kiswahili cha Bujumbura hujitofautisha na Kiswahili cha Kivu katika kuashiria ukubwa usio wa kawaida au/na udunishaji wa nomino kwa hutumia kiambishi ngeli cha ngeli ya 7 na ya 8 ({*ki-bi*}) (mf. *kitoto><bitoto, kinyumba><binyumba*).

Kutokana na maelezo hapo juu, kigezo cha ulinganishaji kimeonesha kuwa miundo ya nomino katika Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu hufanana kwa kiasi kikubwa. Hii ina maana kuwa uambishaji wa nomino kwa viambishi ngeli unafanana kwa kiasi kikubwa na kutofautiana kidogo tu. Ingawa Kiswahili cha Bujumbura kimedhihirisha tofauti ndogo za kimofolojia kwa kutotumia baadhi ya viambishi ngeli vyenye asili ya Kiswahili cha Kivu, hali hiyo haijazuia kueleweka kwa aina hizo mbili za Kiswahili. Hivyo, kwa kuzingatia nadhariatete ya ndugu na ndugu wa mbali, ni wazi kuwa Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu ni ndugu wa karibu.

5.2 Muundo wa Kitenzi katika Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu

Katika tungo, hasa sentensi, kitenzi ni neno linalotoa taarifa kuhusu tendo linalofanyika, lililofanyika au litakalofanyika (Matinde, 2018). Katika muundo msingi wa kitenzi cha Kiswahili, kuna mpangilio na mfuatano maalumu wa vipashio vya kitenzi ambavyo vinashikishwa katika mzizi, yaani kabla na baada yake (Meeussen, 1967; Mutaka na Tamanji, 2000; Nurse, 2008; Matinde, 2018). Katika sehemu hii, watafiti walichunguza na kulinganisha miundo ya vitenzi vya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu kwa ajili ya kutambua na kubainisha upekee

wa kimofolojia wa kitenzi cha Kiswahili cha Bujumbura kwa kuzingatia sifa zinazodhihirisha tofauti za uambishaji na unyambuaji.

5.2.1 Muundo wa Kitenzi katika Kiswahili cha Bujumbura

Muundo wa kitenzi cha Kiswahili cha Bujumbura ulichunguzwa kwa kuchambua na kufafanua data zilizopatikana kutoka katika maeneo teule ya jiji la Bujumbura. Mifano ifuatayo ni baadhi ya sentensi zilizochunguzwa ili kutambua muundo wa kitenzi cha Kiswahili cha Bujumbura kwa kuonesha viambishi awali na tamati vinavyoshikishwa kwenye mzizi wa kitenzi.

1. (a) *Nimezariwa* hapahapa kata ya Kinama.
   (b) Leo *batakushoreya* kesho *habakushoreye*.
   (c) Kazi yangu *inanisayidiya* vitu vingi sana.
   (d) … na *ukapata* gisi *unataka*.

Katika sentensi 1(a-d), muundo wa vitenzi unadhihirisha kuwapo kwa viambishi mbalimbali vinavyotangulia mzizi wa kitenzi. Hivyo, katika vitenzi *nimezaliwa* {*ni*-me-za-riw-a}, *batakushoreya* {*ba*-ta-ku-shor-e-(y)a}, *inanisadiya* {*i*-na-sayidi-(y)a} na *ukapata* {*u*-ka-pat-a}, viambishi {*ni*-}, {*ba*-}, {*i*-} na {*u*-} ni viambishi awali vinavyowakilisha mtenda wa jambo. Pia, vitenzi hivyo huwa na viambishi {-*me*-} [1(a)], {-*ta*-} [1(b)], {-*na*-} [1(c)] na {*ka*-} [1(d)] ambavyo dhima yake ni kuashiria wakati na hali ya kitenzi. Hivyo, {-*me*-} [1(a)] inaashiria wakati uliopita, {-*ta*-} [1(b)] wakati ujao, {-*na*-} [7(c)] wakati uliopo, ilhali kiambishi {-*ka*-} [1(d)] huwakilisha hali ya mfululizo wa matendo.

2. (a) wagonjwa ambawo *tunawapokeya* na watu ambawo tunawapokeya.
   (b) Leo *batakushoreya* kesho *habakushoreye*.
   (c) Tena nikipata hayo mahera *nitawasayidiya* wingine hawana kitu.
   (d) Ndani ya mayisha yangu, *ninayipenda* siyasa.

Katika vitenzi vya sentensi 2(a-d) kumejitokeza viambishi awali vyenye dhima ya kuwakilisha yambwa au yambiwa. Hivyo, katika vitenzi *tunawapokeya* {tu-na-*wa*-poke-(y)a}, *batakushoreya* {ba-ta-*ku*-shore-(y)a}, *nitawasayidiya* {ni-ta-*wa*-sayidi-(y)a}, *ninayipenda* {ni-na-*(y)i*-pend-a} viambishi {-*wa*-} ([2(a)], [2(c)]) na {-*(y)i*-} [2(d)] ni viambishi yambwa vinavyoashiria mtendwa wa jambo, ilhali {-*ku*-} [2(b)] ni kiambishi yambiwa chenye mofimu ya mtendewa jambo.

3. (a) Kwa kile chochote kidogo ambacho *tunachopata* tunamshukuru Mungu.
   (b) Mimi hamna kitu *ninachokifanya.*
   (c) Ni kwa juu mzazi mama *aliponizaa* ndo sehemu anapoishi.
   (d) Naweza kukwambiya suala la *wanavyozungumza* mawese ya bigazi.

Katika sentensi 3(a-d), muundo wa vitenzi unatambulika kuwa na viambishi awali vya urejeshi. Hivyo, katika vitenzi *tunachopata* {tu-na-*cho*-pat-a}, *ninachokifanya* {ni-na-*cho*-ki-fany-a}, *aliponizaa* {a-li-*po*-ni-za-a} na *wanavyozungumza* {wa-na-*vyo*-zungumz-a}, viambishi {-*cho*-} [3(a-b)], {-*po*-} [3(c)] na {-*vyo*-} [3(d)] ni viambishi awali vinavyoashiria urejeshi.

4. (a) Leo batakushoreya kesho *(h)abakushoreye*.
   (b) Bado, *sijawowa*.
   (c) Vijana ambao *(h)awapendi* kazi?
   (d) Nashukuru nimefikia umuri wa namna hiyi *sijapatikana* kuiba ...

Katika sentensi (a-d) kumetokea viambishi vinavyodhihirisha ukanushi. Hivyo, katika sentensi 4(b/d), katika vitenzi *sijawowa* {si-ja-(w)o-(w)a} na *sijapatikana* {*si*-ja-pat-ikan-a}, kiambishi {*si*-} kimetumika kikisimamia ukanushi kwa nafsi ya kwanza umoja. Vilevile, katika vitenzi vya sentensi 4(a) *(h)abakushoreye* {*(h)a*-ba-ku-shorey-e} na 4(d) *(h)awapendi* {*(h)a*-wa-pend-i}, kiambishi {*(h)a*-} ([4(a); 4(d)]) kimesimamia hali ya ukanushi. Tofauti na kiambishi {*si*-} kinachotumika katika nafsi ya kwanza umoja tu, kiambishi {*(h)a*-} hutumika kwa nafsi zingine zote.

5. (a) *Nimezariwa* hapahapa kata ya Kinama.
   (b) *Ninajiperekaga* mimi mwenyewe ku masomo.
   (c) *Niribadirisha* kucheka; sasa niko mutu mukari porepore.
   (d) Na kuyitwangatwanga mpaka *irayinike*.
   (e) … mi nilikuwa *sipendagi* kwanza kutawaliwa.

Licha ya viambishi awali, muundo wa kitenzi cha Kiswahili cha Bujumbura hudhihirisha ujitokezaji wa viambishi tamati. Hivyo, katika vitenzi *nimezariwa* {ni-me-za-*riw*-a} [5(a)], *niribadirisha* {ni-ri-badir-ish-a} [5(c)] na *irayinike* {i-rayin-*ik*-e} [5(d)], viambishi {-*riw*-}, {-*ish*-} na {-*ik*-} ni viambishi nyambulishi ambapo kiambishi {-*riw*-} kinaashiria kauli ya kutendwa, na {-*ik*-} kauli ya kutendeka ilhali kiambishi nyambulishi {-*ish*-} kinaashiria utendeshi. Pia, katika kitenzi *ninajiperekaga* {ni-na-ji-perek-*ag*-*a*} [5(b)] kumedhihirika kiambishi {-*ag*-} ambacho hutumika pamoja na kiambishi cha njeo ya wakati uliopo {-*na*-} (…-*na*-…-*ag*-...) ili kuashiria hali ya mazoea. Vilevile, miongoni mwa viambishi tamati kumejitokeza viambishi tamati mwisho {-*a*}, {-*i*} na {-*e*} ambapo {-*i*} (*sipendagi* {si-pend-ag-*i*} [5(e)]) na {-*e*} (*irayinike* {i-rayin-ik-*e*} [5(d)]) vinaashiria ukanushi katika wakati uliopo.

5.2.2 Muundo wa Kitenzi katika Kiswahili cha Kivu

Katika Kiswahili cha Kivu, viambishi awali na tamati vinavyoshikishwa kwenye mzizi huwa katika utaratibu maalumu na kuwa na dhima tofauti. Sentensi zifuatazo ni mifano iliyotoka katika Kiswahili cha Kivu na ambazo vitenzi vyake vinaonesha viambishi hivyo.

6.(a) Muti *inanguka*.

(b) Siye *tulibachokoza* batoto.
(c) *Anakatala* kubalamukia bazazi yake.
(d) Yenapata majaribu *anapoteya* batoto banakufa.

Sentensi 6(a-d) zilizotolewa kutoka Kiswahili cha Kivu huwa na vitenzi vyenye miundo inayofanana. Katika sentensi hizo, vitenzi *inanguka* {i-na-anguk-a}, *tulibachekoza* {tu-li-ba-chekoz-a}, *anakatala* {a-na-kata-(l)a} na *anapoteya* {a-na-pote-(y)a} vina viambishi awali vilivyopangwa kwa namna sawa na kuwa na dhima sawa. Hivyo, kabla ya mzizi wa kitenzi kumetokea viambishi awali mtenda {i-} [6(a)], {tu-} [6(b)], {a-} [6(c)] na {a-} [6(d)] ambavyo vimewakilisha mtenda wa jambo.

7.(a) *Mitacheza* sana.
(b) *Minakatala* kwenda mu soko.
(c) *Wetafika* saha gani ?
(d) *Yenapata* majaribu anapoteya batoto banakufa.
(e) *Ntafanya* siku ingine.

Katika mifano hiyo juu, kumetambulika ufupishaji wa viwakilishi vya nafsi ili kushikamana na viambishi vingine kwenye mzizi wa kitenzi. Hivyo, katika sentensi 7(a-d), vitenzi *mitacheza* {mi(ye)-Ø-ta-chez-a}, *minakataa* {mi(ye)-Ø-na-kata-a}, *wetafika* {we(ye)-Ø-ta-fik-a} na *yenapata* {ye(ye)-Ø-na-pat-a} vimedhihirisha miundo inayohusisha viwakilishi vya nafsi *miye, weye* na *yeye* vilivyofupishwa na kuwa viambishi vya nafsi {mi-} [7(a); 2(b)], {we-} [7(c)] na {ye-} [7(d)] ambavyo vimechukua nafasi ya viambishi vya nafsi ya kwanza {ni-}[7(a); 7(b)], pili {u-} [7(c)] na tatu {a-} [7(d)] katika umoja. Vilevile, katika Kiswahili cha Kivu, muundo wa vitenzi umedhihirisha ufupishaji wa kiambishi cha nafsi kikifuatwa na kiambishi {-ta-} cha njeo ya wakati ujao. Kwa mfano, kiambishi cha nafsi ya kwanza umoja {ni-} hufupishwa na kuwa {n-} (*ntafanya* {*n*-ta-fany-a}) [7(e)].

8.(a) Muti *inanguka*.
(b) Sisi *tunabachokoza* batoto.
(c) *Anakatala* kubalamukiya bazazi yake.
(d) Yenapata majaribu *anapoteya* batoto banakufa.
(e) Mu camp *kulikuwa* bunyumba.
(f) *Balianzaka* kulima vile.
(g) Jana *miliuza* kitu mingi.
(h) *Mitacheza* sana.
(i) *Ntafanya* siku ingine.

Katika sentensi hapo juu, muundo wa vitenzi vya Kiswahili cha Kivu umedhihirisha kuwapo kwa viambishi vinavyowakilisha njeo za wakati. Hivyo, kiambishi cha njeo ya wakati uliopo {-na-} kimejitokeza katika vitenzi vya sentensi 8(a) (*inaanguka* {i-*na*-anguk-a}), 8(b) (*tunabachokoza* {tu-*na*-ba-chokoz-a}), 8(c) (*anakatala* {a-*na*-

kata-(l)a}) na sentensi 8(d) (*anapoteya* {a-*na*-pote-(y)a}). Pia, katika sentensi 8(e-i), miundo ya vitenzi *kulikuwa* {ku-*li*-ku-w-a}, na *miliuza* {mi-*li*-uz-a}; *mitacheza* {mi(ye)-Ø-*ta*-chez-a}, *ntafanya* {n-*ta*-fany-a} imeweka wazi matumizi ya viambishi vya wakati uliopita {-li-} na wakati ujao {-ta-} katika Kiswahili cha Kivu.

9.(a) *Nimezaliwa* katika nchi ya DRC.
(b) Kongo *nimeishi* pale Uvira.
(c) *Minaisha* kupakala mafuta.
(d) Alikuwa *aliisha enda*/ *kwenda*.

Katika sentensi 9(a-b), muundo wa vitenzi *nimezaliwa* {ni-*me*-za-liw-a} na *nimeishi* {ni-*me*-ishi} umeshirikisha kiambishi awali {-me-} kilichotumika kuonesha hali timilifu katika Kiswahili cha Kivu. Pia, kiambishi {-me-} huashiria wakati uliopita kama katika *nimezaliwa* {ni-*me*-za-liw-a} kwa maana ya {-li-}. Vilevile, hali hiyo inaweza kuoneshwa na kitenzi -*isha* kama inavyoonekana katika sentensi 9(c) (*minaisha* {mi(ye)-na-ish-a}) na 9(d) (*aliisha* {a-li-ish-a}). Katika muktadha huo, kitenzi -*isha* hutumika kama kitenzi kisaidizi huku kikishirikiana na kitenzi kikuu (*Minaisha* kupakala; *aliisha* enda/ kwenda).

10.(a) *Sipende* mambo aya.
(b) *Abaandike* mambo aya.
(c) Bazazi *abaseme* mambo mingi.
(d) *Abataenda* kura nani, kura nkuku.
(e) Iyi kilianguka, lakini kile *akikuanguka.*

Katika sentensi za Kiswahili cha Kivu hapo juu, miundo ya vitenzi inadhihirisha ukanushi kupitia viambishi awali vinavyoonesha hali hiyo. Hivyo, katika sentensi 10(a), kiambishi {si-} (*sipende* {*si*-pend-e}) kimetumika kuwakilisha ukanushi katika nafsi ya kwanza umoja. Pia, katika sentensi 10(b-e), kiambishi {a-} (*abaseme* {*a*-ba-sem-e}, *abataenda* {*a*-ba-ta-end-a}, *akikuanguka* {*a*-ki-ku-anguk-a}) huonesha ukanushi kwa nafsi zingine zote.

11.(a) *Niliyimutumiya* juzi.
(b) Sisi *tunabachokoza* batoto.
(c) Anakatala *kubalamukiya* bazazi yake.

Katika sentensi 11(a-c), kwenye vitenzi *niliyimutumiya* {ni-li-*yi*-*mu*-tum-i-(y)a}, *tunabachokoza* {tu-na-*ba*-chokoz-a} na *kubalamukiya* {ku-*ba*-lamuki-(y)a} kumetokea viambishi awali ambavyo dhima yake ni kuwakilisha yambwa au yambiwa. Hivyo, kiambishi {-(y)i-}, {-mu-} [11(a)], {-ba-} [11(b)] na {-ba-} [11(c)] ni viambishi vinavyowakilisha yambwa ambapo {-mu-} [11(a)] ni kinawakilisha yambiwa.

12.(a) *Nilizoweyaka kumutembeleya* ule kiyana.
(b) Katika kazi kilimo, walimaji *awatumikishake* mashini, ila majembe.
(c) Kuzaliwa kwangu, *nilizaliwa* Kongo.

(d) Miye *nilikuwaka* mugonjwa.

Katika sentensi 12(a-d), kwenye vitenzi *nilizoweyaka* {ni-li-zowe-*(y)ak*-a}*, kumutembeleya* {ku-mu-tembe-*le*-(y)a}*, awatumikishake* {a-wa-*tum*-*ik*-*ish*-*ak*-e}*, nilizaliwa* {ni-li-za-*liw*-a}*, nilikuwaka* {ni-li-ku-w-*ak*-a}, kumetokea viambishi tamati kila mara baada ya mzizi. Hivyo, viambishi {-*le*-} [12(a)], {-*ik*-} [12(b)], {-*ish*-} [12(b)], na {-*liw*-} [12(c)] ni viambishi nyambulishi vinavyoashiria kauli ya kutendea [12(a)], ya kutendeka [12(b)], ya kutendesha [12(b)], na ya kutendewa [12(c)] mtawalia. Pia, katika vitenzi vya sentensi 12(a-b/d) kumetokea kiambishi tamati {-*ak*-} ambacho kimeungana na mofu za njeo ya wakati uliopo {-*na*-} ({-*na*-…-*ak*-}) na wakati uliopita {-*li*-} ({-*li*-…-*ak*-}) ili kuonesha uzoefu wa tendo kutokea katika wakati wa sasa, wakati uliopita na wakati ujao ({-*ta*-…-*ak*-}) (mf. Kila siku, wanafunzi *watafikaka* busubuyi.). Vilevile, katika vitenzi vya sentensi 12(a-d), kumejitokeza viambishi tamati mwishoni ambavyo ni {-*a*-} [12(a/c-d)] na {-*e*-} [12(b)].

Kutokana na maelezo hapo juu, muundo wa kitenzi cha Kiswahili cha Kivu umedhihirisha ujitokezaji wa viambishi awali na tamati vyenye dhima tofauti. Hivyo, muundo wa kitenzi cha Kiswahili cha Kivu hufuata kanuni za mpangilio wa viambishi vinavyounda kitenzi cha Kibantu (Meeussen, 1967; Mutaka na Tamanji, 2000; Nurse, 2008 na Matinde, 2018).

5.2.3 Ulinganishi wa Muundo wa Kitenzi cha Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu

Katika sehemu 5.2.1 na 5.2.2 miundo ya vitenzi katika Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu imebainishwa na kujadiliwa. Kwa kutumia kigezo cha ulinganishaji na kuzingatia nadhariatete ya ndugu na ndugu wa mbali, yapo mambo kadhaa yanayodhihirika. Kwa upande mmoja, imebainishwa kuwa vitenzi vya Kiswahili cha Bujumbura huwa na viambishi awali vya nafsi, vya njeo na viambishi yambwa au yambiwa, sawa na Kiswahili cha Kivu. Vilevile, vitenzi vya Kiswahili cha Bujumbura huwa na viambishi tamati, yaani vinyambulishi na viishio, kama ilivyo katika Kiswahili cha Kivu.

Kwa upande mwingine, uambishaji wa vitenzi katika Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu umeonesha tofauti fulani. Pale ambapo Kiswahili cha Bujumbura hutumia viambishi awali mtenda (*nitacheza* {<u>*ni*</u>-ta-chez-a}; *anapata* {<u>*a*</u>-na-pat-a}), Kiswahili cha Kivu hufupisha kiwakilishi cha nafsi na kutumiwa kama kiambishi cha nafsi (awali mtenda) (mf. *mitacheza* {<u>mi(ye)</u>-Ø-ta-chez-a} [2(b)], *yenapata* {<u>ye(ye)</u>-Ø-na-pat-a} [2(d)]). Pia, katika Kiswahili cha Bujumbura kuna viambishi ambavyo havihusiki katika Kiswahili cha Kivu. Hivyo, katika kuashiria hali ya kuendelea kwa tendo, Kiswahili cha Bujumbura hutumia kiambishi {-*na*-} (ninarima) ilhali Kiswahili cha Kivu hutumia {-*ko*-…-*na*-} (ekonalima). Aidha, ambapo muundo wa Kiswahili cha Bujumbura unakubali viambishi rejeshi (-o- rejeshi) kama vile {-*cho*-} katika *ninachokifanya* {ni-na-*cho*-ki-fany-a} [10(b)],

na {-*po*-} katika *aliponizaa* {a-li-*po*-ni-za-a} [10(c)], Kiswahili cha Kivu hutumia kipashio -*enye* ambacho kina sifa ya kisintaksia kwani huingia katika muundo wa sentensi (mf. Batu *benye* banacheza ni binamu zangu = wanaocheza). Vilevile, katika Kiswahili cha Bujumbura kuna kiambishi tamati {-*ag*-} (mf. *ninajiperekaga* {ni-na-ji-perek-*ag*-*a*} [12(b)], *sipendagi* {si-pend-*ag*-i} [12(e)]) ambacho hutofautiana na kile cha Kiswahili cha Kivu katika matamshi; huwa {-*ak*-} (*balianzaka* {ba-li-anz-*ak*-a} [3(f)]). Tofauti nyingine imejitokeza katika ukanushi ambapo Kiswahili cha Bujumbura hutumia kiambishi mwisho {-*i*-} katika wakati uliopo (mf. *sipendagi* {si-pend-*ag*-i} [12(e)]), ilhali Kiswahili cha Kivu hutumia kiambishi mwisho {-*e*-} (mf. *sipende* {si-pend-*e*} [5(a)]), *abaandike* {a-ba-andik-*e*} [5(b)], *abaseme* {a-ba-sem-*e*} [5(c)]).

Kutokana na maelezo hapo juu, uambishaji wa vitenzi na dhima ya viambishi vilivyoshikishwa kwenye mzizi wa kitenzi umedhihirisha undugu wa karibu wa Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu kwa sababu watumiaji wa pande zote mbili husikilizana na kuelewana.

5.3 Kanuni za Kimofosintaksia katika Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu

Kanuni za kimofosintaksia zinaongoza uwiano wa maneno yaundayo tungo. Kanuni hizo ni sheria za kiisimu zenye dhima ya kueleza uhusiano uliopo baina ya vipashio vya kimofolojia na kisintaksia zinazoelekeza na kufafanua usahihi katika matumizi ya lugha (Dubois, 2000; Oichoe, 2005; Barno, 2013; Mulei na wenzake, 2021; Mulei, 2023). Hivyo, katika sehemu hii, watafiti walilinganisha kanuni za kimofosintaksia baina ya Kiswahili cha Kivu na Kiswahili cha Bujumbura, kwa kuchunguza upatanisho wa kisarufi unavyojitokeza baina ya nomino na vitenzi au nomino na vivumishi. Jambo hilo liliwaelekeza kutambua ufanano na utofauti baina ya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu, na hivyo, kuelewa upekee wa kimofolojia wa Kiswahili cha Bujumbura.

5.3.1 Kanuni za Kimofosintaksia katika Kiswahili cha Bujumbura

Kama ilivyo kawaida ya lugha za Kibantu, nomino ya Kiswahili cha Bujumbura iliyopo katika sentensi ndiyo inayoongoza uwiano wa baadhi ya vipashio vya kisarufi vilivyomo kwenye sentensi. Uchunguzi wa data ulionesha kuwa vitenzi na vivumishi vinavyoandamana na nomino kwenye sentensi huwa na vipatanishi vya ngeli kutokana na hiyo nomino.

13.(a) Tena *(mimi) nikipata* hayo mahera nitawasayidiya *wingine hawana* kitu.
(b) *Baba mwenyewe anaponizaa* anaishi Burundi.
(c) *(Sisi) turiwahi* kwenda, na ta ivi tunayendaga.
(d) Kuna *(watu) wanaoendesha* shughuli tofauti za maendeleo.

Katika sentensi 13(a-b), ambapo sentensi zilizotolewa zimehusisha nafsi ya kwanza na ya tatu umoja, kiwakilishi cha nafsi *mimi* na nomino *baba* vimeungana na vitenzi *nikipata* {*ni*-ki-pat-a} na *anaponizaa* {*a*-na-po-ni-za-a}. Mifano hii imeonesha kuwa kanuni za kimofosintaksia zimezingatiwa. Katika sentensi 13(a), kiwakilishi *mimi* kimewiana na kitenzi *nikipata* kupitia kiambishi cha nafsi {*ni*-}, ilhali nomino *baba* imepatana na kitenzi *anaponizaa* kwa kiambishi nafsi {*a*-}. Pili, katika sentensi 13(c-d) ambapo kumetumiwa nafsi za wingi, kiwakilishi *sisi* kimehusishwa na kitenzi *turiwahi* {*tu*-ri-wah-i} kwa kiambishi nafsi {*tu*-}, ilhali nomino *watu* imeungana na kitenzi *wanaoendesha* {*wa*-na-o-end-esh-a} kwa kiambishi nafsi {*wa*-}.

14.(a) *Mitihani* ni lazima *iwepo* kutokana na magonjwa.
(b) *Bitu binayenda* binapanda.
(c) *Kazi yangu inanisayidiya* vitu vingi sana.
(d) *Mawese yanachukuriwa*… yanachujwaaa…

Katika sentensi za Na. 14 kumeoneshwa namna nomino kutokana na ngeli mbalimbali zinavyoungana na kitenzi. Hivyo, katika sentensi 14(a) nomino *mitihani* ya ngeli ya U-I imewiana na kitenzi *iwepo* {*i*-w-e-po} kwa kiambishi ngeli {*i*-}, ilhali katika 14(b) nomino *bitu* ya ngeli ya KI-BI(VI) imepatana na kitenzi *binayenda* {*bi*-na-(y)end-a} kwa kiambishi {*bi*-}. Pia, katika 14(c) nomino *kazi* ya ngeli ya I-ZI imewiana na kitenzi *inanisayidiya* {*i*-na-ni-sayidi-(y)a} kwa kiambishi {*i*-}. Vilevile, katika sentensi 14(d), nomino *mawese* ya ngeli ya (LI)-YA imewiana na kitenzi *yanachukuriwa* {*ya*-na-chuku-riw-a} kwa kiambishi ngeli kipatanishi {*ya*-}.

15.(a) Mimi niko na *mudogo wangu*, nina mama nina baba.
(b) Ni lazima ile *mizozo midogomidogo* itokeye kwenye jamii.
(c) Wanaweka mataa juu ya boti, … na *fasi yote.*
(d) Naweza kusema *mambo machache*; siyo *mambo mengi* lakini.

Katika sentensi za 15 kumetolewa nomino na vivumishi vilivyoandamana nazo. Katika sentensi 15(a-b), nomino *mudogo* ya ngeli ya A-BA na nomino *mizozo* ya ngeli ya U-I zimeambatana na vivumishi *wangu* {*a*-angu} na *midogomidogo* {*mi*-dogo-*mi*-dogo} kwa viambishi ngeli {*a*-} [15(a)] na {*mi*-} [15(b)]. Pia, katika sentensi 15(c), nomino *fasi* ya ngeli ya I-ZI imeambatana na kivumishi *yote* {*i*-ote} kwa kiambishi ngeli {*i*-} [15(c)]; ilhali, katika sentensi 15(d), nomino *mambo* ya ngeli ya LI-YA imewiana na kivumishi *machache* {*ma*-chache} na *mengi* {*ma*-ingi} kwa kiambishi ngeli {*ma*-}.

5.3.2 Kanuni za Kimofosintaksia katika Kiswahili cha Kivu

Katika sehemu hii, watafiti walichunguza namna nomino na vitenzi, na nomino na vivumishi vinavyoandamana katika tungo au sentensi ya Kiswahili cha Kivu; na

kanuni za kimofosintaksia zinazotumika katika mchakato mzima wa kutungia tungo za aina mbalimbali.

16.(a) *(Miye) minasema* …
(b) Aba *bafilles (siye/shiye) tukonaona banazunguluka* (h)umu.
(c) *Baba yangu aligonjwa* miaka mingi sana.
(d) *Mimi nilisomeya* Goma, nashindwaka kukoprendre …

Katika sentensi 16(a) na 16(c-d), kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja *miye* na nomino *baba* hupatana na vitenzi *minasema* {*mi(ye)*-Ø-na-sem-a}, *aligonjwa* {*a*-li-gonjw-a} na *nilisomeya* {*ni*-li-som-e-(y)a} kwa viambishi {*mi*-} [16(a)], {*a*-} [16(c)] na {*ni*-} [16(d)]. Vilevile, katika sentensi 16(b), kiwakilishi cha nafsi ya kwanza wingi *siye/shiye* na nomino *bafilles* vimeungana na vitenzi *tukonaona* {*tu*-ko-na-on-a}) na *banazunguluka* {*ba*-na-zunguluk-a}) kwa viwakilishi vya nafsi ya kwanza wingi {*tu*-} na ya tatu wingi {*ba*-}.

17.(a) *Meno inatoka*.
(b) *Mafuriko ilitokeya* nyumba yetu ikayala mayi.
(c) *Bitu bikaharibika* mu nyumba, …
(d) *Sauti* yangu *ayibadilike.*

Katika mifano ya kundi Na. 17, tungo zilizotolewa zinaonesha ushirikiano baina ya nomino za ngeli tofauti na vitenzi, na kanuni za kimofosintaksia zinazotumika. Kwa upande mmoja, katika sentensi 17(a-b), nomino *meno* (ngeli ya LI-YA) na *mafuriko* (ngeli ya (LI)-YA) zimeungana na vitenzi *inatoka* {*i*-na-tok-a}*, ilitokeya* {*i*-li-toke-(y)a} kwa kiambishi kipatanishi cha ngeli {*i*-} ambacho kwa kawaida ni cha ngeli ya I-ZI. Upande mwingine, nomino *sauti* ya ngeli ya I-ZI imeunganishwa na kitenzi *ayibadilike* {a-*(y)i*-badil-ik-e}) kwa kiambishi ngeli {*(y)i*-}.

18.(a) Uko d'accord na *(h)iyi mambo* ekonasema?
(b) *Mama yangu* yiko na mutu yiko na *dada zangu*.
(c) Ni hizi hali za *usalama mudogo*.
(d) *Kiti moya*, *viti mbili*, …

Sentensi hizi Na. 18 zinadhihirisha namna nomino zinavyoshirikiana na vivumishi. Katika sentensi 18(a-c), nomino *mambo*, *mama, dada* na *usalama* zimeambatana na vivumishi *(h)iyi* {i-*(y)i*}), *yangu* {*a*-angu}, *zangu* {*zi*-angu} na *mudogo* {*mu*-dogo} kwa viambishi {-*(y)i*} [18(a)], {*a*-} [18(b)], {*zi*-} [18(b)] na {*mu*-} [18(c)]. Pia, katika sentensi 18(e), nomino *kiti* na *viti* zimeandamana na vivumishi *moya* {*Ø*-moya} na *mbili* {$Ø_1$-N_2-(b)ili}), ambapo upatanisho wa kisarufi umekaliwa na kiambishi kapa.

5.3.3 Ulinganishi wa Kanuni za Kimofosintaksia katika Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu

Katika sehemu 5.3.1 na 5.3.2 zimebainishwa na kufafanuliwa kanuni za kimofosintaksia zinazofanya kazi katika Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha

Kivu. Imebainishwa namna mofu zinavyotumika kufanikisha uwiano wa maneno yanayoandamana katika mfumo wa tungo au sentensi. Kwa kuzingatia misingi ya ulinganishaji na nadhariatete ya ndugu na ndugu wa mbali, imedhihirika kuwa kanuni za kimofosintaksia baina ya nomino au viwakilishi vyake na vitenzi au vivumishi hutumika kwa namna sawa baina ya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu.

Kwanza, katika matumizi ya viwakilishi nafsi au nomino zinazowakilishwa navyo, Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu hutumia kanuni sawa za kimofosintaksia. Hivyo, Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu hujenga upatanisho wa kisarufi baina ya viwakilishi vya nafsi au nomino hizo na vitenzi vinavyoandamana navyo kwa kutumia viambishi nafsi {ni-/n-}, {u-}, {a-}, {tu-}, {m-} na {ba-/wa-}. Hata hivyo, kwa upande huo, Kiswahili cha Bujumbura hulazimisha ujitokezaji wa viambishi nafsi (mf. mimi *ninasema* {*ni*-na-sem-a}; wewe *utafika* {*u*-ta-fik-a}; yeye *anapata* {*a*-na-pat-a}) pale ambapo Kiswahili cha Kivu hukibadilishana na sehemu ya kiwakilishi nafsi (mf. *minasema* {*mi(ye)*-Ø-na-sem-a} [16(a)] ; *wetafika* {we(ye)-Ø-ta-fik-a} [2(c)] ; *yenapata* {ye(ye)-Ø-na-pat-a} [2(d)]). Vilevile, nomino za Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu zinazotokana na ngeli fulani huweza kuoanishwa na vitenzi na upatanisho wa kisarufi ukikaliwa na viambishi vipatanishi vya ngeli. Katika muktadha huu, tofauti baina ya aina hizo mbili za Kiswahili hubainika pale ambapo Kiswahili cha Bujumbura hulazimisha ujitokezaji wa kiambishi kipatanishi cha ngeli kutokana na nomino husika ilhali katika Kiswahili cha Kivu mofu {i-} inaweza kusimamia ngeli zozote (mf. meno *inatoka* {*i*-na-tok-a} [17(a)], mafuriko *ilitokeya* {*i*-li-tok-e-(y)a} [17(b)]).

Pili, katika mfumo wa tungo za Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu, nomino inaweza kuandamana na kivumishi. Katika muktadha huu, tofauti ndogo baina ya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu imedhihirika kwani nomino yoyote ya Kiswahili cha Bujumbura huambatana na kivumishi kwa kiambishi ngeli kinachotokana na ngeli ya nomino (mf. Kiti *kimoja* {*ki*-moja}, Viti *viwili* {*vi*-ili}), ilhali nomino ya Kiswahili cha Kivu huweza kuandamana na kivumishi bila kuoanishwa na kiambishi ngeli chochote (mf. kiti *moya* {*Ø*-moya} [18(d)]); viti *mbili* {$Ø_1$-N_2-(b)ili}) [18(d)]).

Ingawa kumeonekana tofauti fulani, maelezo hayo juu ya kanuni za kimofosintaksia kati ya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu yamedhihirisha ufanano mkubwa baina ya aina hizo mbili za Kiswahili. Kwa mantiki hiyo, Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu huwa na unasaba wa kindugu.

6.0 Hitimisho

Utafiti huu umelinganisha mofolojia ya Kiswahili cha Bujumbura na cha Kivu ili kutambua upekee wa kimofolojia wa Kiswahili cha Bujumbura. Hivyo, kwa

kutumia misingi ya ulinganishaji na kuzingatia nadhariatete ya ndugu na ndugu wa mbali, uchunguzi na ufafanuzi wa kimaumbo wa nomino na vitenzi, na uchunguzi wa kanuni za kimofosintaksia ulionesha kuwa hakuna tofauti ya msingi baina ya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu. Kuna ufanano wa muundo wa nomino ya Kiswahili cha Bujumbura na nomino ya Kiswahili cha Kivu. Viambishi ngeli hushirikiana na mashina ili kukamilisha muundo wa nomino vikionesha ama umoja na wingi au udogo na ukubwa kwa namna sawa. Katika muktadha huu, Kiswahili cha Bujumbura hakitumii viambishi ngeli {*bu-*} na {*hi-*} vinavyodhihirisha udogo katika Kiswahili cha Kivu. Pili, kuhusu uambishaji wa vitenzi, Kiswahili cha Bujumbura hutofautiana na Kiswahili cha Kivu kwa kutohusisha ufupishaji wa kiwakilishi cha nafsi wala kukitumia badala ya kiambishi nafsi. Tatu, kuhusu matumizi ya kanuni za kimofosintaksia, nomino na vitenzi, na nomino na vivumishi vya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu hushirikiana kwa viambishi nafsi au viambishi vipatanishi vya ngeli. Katika muktadha huu, aina zote mbili zimedhihirisha ufanano isipokuwa pale Kiswahili cha Bujumbura kinapohusisha viambishi nafsi na viambishi vipatanishi vya ngeli vinavyosimamia uwiano wa vipashio vya tungo ilhali vinafupishwa katika Kiswahili cha Kivu. Kutokana na matokeo hayo, kufanana kwa sifa za kimofolojia baina ya Kiswahili cha Bujumbura na Kiswahili cha Kivu ndiko kunakotawala, hali ambayo imedhihirisha undugu wa karibu wa aina hizo mbili za Kiswahili. Hata hivyo, Kiswahili cha Bujumbura hujijengea upekee wa kimofolojia kwa kutofautiana na Kiswahili cha Kivu kwa baadhi ya sifa. Hivyo, kuna haja pia ya kulinganisha Kiswahili cha Bujumbura na lahaja zingine za Kiswahili cha Kongo ili kuendelea kutafiti uwepo wa lahaja za kipekee nchini Burundi.

Marejeleo

Ali, S. F. (2015). *Tofauti ya Msamiati wa Lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini.* Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Barno, C. (2013). "Muundo wa Kimofosintaksia wa Kitenzi cha Kinandi kwa Mutazamo wa Kiyunzi cha Kanuni Finyu." *Nordic Journal of African Studies,* 22(4), 213-235.

Benabou, A. (1982). Recherches sur le swahili du Burundi : Les nominaux. Thèse de doctorat (Non publié). Université de Nice l.

Bizongwako, L. (1985). Evolution sociolinguistique de la ville de Bujumbura, de 1950 à 1984. Mémoire de licence (Non publié). Université du Burundi.

Bose, P. B. na Nassenstein, N. (2016) Morphosyntactic Core Features of Kivu Swahili: A Synopsis. *Afrikanistik-Äegyptologie Online*. https://www.afrikanistik-aegyptologie-online.de/archiv/2016/4479

CRELACS. (2023). *Stratégies pour un aménagement linguistique cohérent au Burundi.* Bujumbura: Université du Burundi.

De Rooij, V. A. (2007). "Grammatical Borrowing in Katanga Swahili." Katika Y. Matras na J. Sakel (Wah.), *Grammatical Borrowing in Cross-Linguistic Perspective.* Berlin : Mouton de Gruyter.

Dubois, J. (2000). *Dictionnaire de Linguistique.* Paris : Larousse.

Ferrari, A., Kalunga, M. na Mulumbwa, G. (2014). *Le Swahili de Lubumbashi. Grammaire, textes, lexique*. Paris: Karthala.

Giles, H. (1982). *Communication Accommodation Theory*. Cambridge: Cambridge University Press.

Giles, H. na Byrne, J. L. (1982). "An Intergroup Approach to Second Language Acquisition". *Journal of Multilingual and Multicultural Development*. 19: 17-40.

Goyvaerts, D. (2007). "Bukavu Swahili: Tense, Aspect and Blurry History." *Journal of Asian and African Studies.* 74: 5-33.

Masebo, J. A. na Nyambari, C. M. (2016). *Nadharia ya Lugha, Kiswahili 1: Kidato cha 5 na 6*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Massamba, D. P. B. (2006). "Kiswahili cha Musoma: Mwanzo wa Lahaja Nyingine ?" *Kiswahili,* 69(3): 24-39.

Massamba, D. P. B. (2007). *Kiswahili Origins and the Bantu Divergence-Convergence Theory*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y.M. na Hokororo, J. I. (2009). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA): Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: TUKI.

Matinde, S. R. (2018). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia: Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) LTD.

Mazunya, M. na Habonimana, A. (2010). *Les Langues de Scolarisation dans l'Enseignement Fondamental en Afrique Subsaharienne Francophone: Cas du Burundi. Résumé Institutionnel du Rapport d''Etude Pays*. Bujumbura: AUF.

Meeussen, A. E. (1967). "Bantu Grammatical Reconstructions." *Africana Lingüística, 3, Annalen Van HEt Koninklijk Museum voor Midden-Afrika*. 61: 79-121.

Moeschler, J. na Auchlin, A. (2000). *Introduction à la Linguistique Contemporaine*. Paris: Armand Colin.

Muaka, L., Nduwamahoro, A. na Butoyi, D. (2024). "Language Policy in Burundi". Katika E. M. Lisanza na L. Muaka (Wah.), *The Palgrave Handbook of Language Policies in Africa.* Switzerland: Springer Nature Switzerland AG. Kur. 140-159. https://doi.org/10.1007/978-3-031-57308-8_6

Mulei, M. (2021). "Uhakiki Linganishi wa Kanuni za Mifanyiko ya Vivumishi vya Luganda na Kiswahili Sanifu." *East African Journal of Swahili Studies*. 6(1): 132-153.

Mulei, M. (2023). "Uhakiki Linganishi wa Kanuni za Mifanyiko ya Vivumishi vya Luganda na Kiswahili Sanifu." *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), 132-153. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

Mulei, M., Ambuyo, B. A. na Amukowa, D. N. (2021). "Mwingiliano wa Kanuni za Kimofosintaksia wa Ngeli Nomino za Luganda katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu." *Mwanga wa Lugha.* 1: 39-50.

Mutaka, N. N. na Tamanji, P. N. (2000). *An Introduction to African Linguistics.* München: LINCOM Europa.

Nassenstein, N. (2017). "Pluractional Marking in Bunia Swahili (Ituri Kingwana)." *STUF*. 70(1): 195-213.

Nassenstein, N. (2015). *Kisangani Swahili. Choices and Variation in a Multilingual Urban Space.* München: LINCOM Europa.

Nassenstein, N. na Bose, P. B. (2016). *Kivu Swahili Texts and Grammar Notes.* München: LINCOM Europa.

Nassenstein, N. na Bose, P. B (2020). "Morphological Features of Kiswahili Youth Language(s): Evidence from Dar es Salaam, Goma, Lubumbashi and Nairobi." *Linguistics Vanguard*. 6(4): 1-13.

Nassenstein, N. na Gerrit J. D. (2020). "Bunia Swahili and Emblematic Language Use." *Journal of Language Contact.* 12: 823-855.

Nassenstein, N. na Shinagawa, D. (2019). "On Variation in Swahili: Current Approaches, Trends and Directions." *Swahili Forum.* 26: 1-45.

Nkwera, F. (1989). *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Novakova, I. (2010). *Syntaxe et Sémantique des Prédicats. Approche contrastive et fonctionnelle*. Grenoble: Université Stendhal.

Nsabimana, J. (1988). Essai d'Interprétation des Emprunts Kirundi au Swahili. Mémoire de Licence (Non publié). Université du Burundi.

Nshimirimana, E., Misago M. J. na Tuyubahe, P. (2022). "Le Système Nominal du Kirundi (Bantou, JD62) et du Kiswahili (Bantou, G42) : Une Analyse Contrastive." *Language in Africa*. 3(1): 57-83. Doi: 10.37892/2686-8946-2022-3-1-57-83

Ntiranyibagira, C. (2017). La Dynamique du Kirundi en Contexte Plurilingue: Pratiques Langagières et Discours Epilinguistiques. Thèse de Doctorat (Non publié). Université Houphouët Boigny.

Nyandago, F. O. (2013). Uchanganuzi Linganishi wa Sintaksia ya Sentensi Sharti ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Nurse, D. na Hinnebusch, T. J. (1993). *Swahili and Sabaki: A Linguistic History*. Berkeley: University of California Press.

Nurse, D. (2008) *Tense and Aspect in Bantu*. New York: Oxford University Press.

Oichoe, M.P. (2005). *Ulinganishi wa Kirai Tenzi cha Kiswahili na Ekegusii Kimofosintaksia: Mtazamo wa Uminimalisti*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Salim, A. S. (2015). Kuchunguza Dhima za Semi Zilizoandikwa kwenye Mikoba Kisiwani Pemba. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Salum, H. M. (2018). *Ulinganishi wa Kifonolojia kati ya Lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu.* Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.